TANGAZO LA SERIKALI NA. 167 la tarehe 10/3/2023

SHERIA YA MAHAKAMA ZA MAHAKIMU,
(SURA YA 11)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini cha 71(1))*

KANUNI ZA UTARATIBU WA MADAI MADOGO ZA MWAKA, 2023

## MPANGILIO WA KANUNI

### SEHEMU YA KWANZA
### MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina.
2. Matumizi.
3. Utekelezaji wa Kanuni.
4. Tafsiri.

### SEHEMU YA PILI
### UFUNGUAJI WA MADAI MADOGO NA MAJIBU

5. Uwasilishaji wa madai madogo.
6. Kukataliwa kwa hati ya madai.
7. Shauri kupangwa kwa hakimu.
8. Upelekaji wa hati ya madai.
9. Kushindwa kupeleka hati ya madai.
10. Majibu ya hati ya madai.
11. Majibu ya madai kinzani.
12. Kushindwa kuwasilisha majibu ya hati ya madai.
13. Maridhiano kwenye madai.

### SEHEMU YA TATU
### USIKILIZWAJI WA SHAURI

14. Kuhudhuria na madhara ya kushindwa kutohudhuria mahakamani.
15. Kutengua hukumu ya upande mmoja na amri ya kutupilia mbali shauri.
16. Usikilizwaji wa shauri.
17. Katazo la maahirisho

SEHEMU YA NNE
HUKUMU NA UTEKELEZAJI WA TUZO

18. Hukumu na tuzo.
19. Gharama.
20. Utekelezaji wa tuzo.

SEHEMU YA TANO
RUFAA NA MAPITIO

21. Utaratibu wa rufaa na mapitio.

SEHEMU YA SITA
MASHARTI YA JUMLA

22. Namna ya kuwasilisha maombi.
23. Ada.

JEDWALI

SHERIA YA MAHAKAMA ZA MAHAKIMU,
(SURA YA 11)

KANUNI

*(Zimetengenezwa chini cha 71(1))*

KANUNI ZA UTARATIBU WA MADAI MADOGO ZA MWAKA, 2022

Jina

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Utaratibu wa Madai Madogo za Mwaka 2022.

Matumizi

2. Kanuni hizi zitatumika wakati mahakama inashughulikia mashauri ya madai madogo isipokuwa-

(a) madai dhidi ya Serikali; na
(b) madai yanayotokana na migogoro ya ardhi, kazi, mirathi, ndoa pamoja na mashauri mengine yaliyowekewa utaratibu mahsusi na sheria nyingine.

Utekelezaji wa Kanuni

3. Katika kutekeleza Kanuni hizi, mahakama itajitahidi-

(a) kurahisisha, kuharakisha na kuweka unafuu wa uendeshaji wa madai madogo; na
(b) kuamua madai kwa kuzingatia haki ya msingi bila kujali masharti ya kiufundi.

Tafsiri

4. Katika Kanuni, hizi isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"hakimu mfawidhi" maana yake ni hakimu mfawidhi wa mahakama;

“mahakama" maana yake ni mahakama ya hakimu mkazi au mahakama ya wilaya;

“Mahakama Kuu” maana yake ni Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

“madai madogo” maana yake ni mashauri yenye asili ya madai yenye thamani isiyozidi shilingi milioni mia moja na yasiyoangukia katika mamlaka ya kifedha ya mahakama ya mwanzo;

"mdai" maana yake ni mtu anayewasilisha madai madogo mahakamani akiwemo mtu yeyote anayekuwa mdaawa wa shauri la madai madogo katika nafasi ya mdai;

"mjibu madai" maana yake ni mtu ambaye madai madogo yamewasilishwa dhidi yake; na

Sura ya 11

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Mahakama za Mahakimu.

## SEHEMU YA PILI
## UFUNGUAJI WA MADAI MADOGO NA MAJIBU

Uwasilishaji wa madai madogo

TS Na. 248 la Mwaka 2018

5.-(1) Madai yatafunguliwa kwa njia ya kielektroniki kwa mujibu wa Kanuni za Ufunguaji wa Mashauri ya Kielektroniki, kwa kuwasilisha hati ya madai inayoshabihiana kwa kadiri iwezekanavyo na Fomu A iliyoainishwa kwenye Jedwali la Kanuni hizi.

(2) Kila hati ya madai itajumuisha madai yote ambayo mdai anastahili ingawa mdai anaweza kuacha au kusamehe sehemu yoyote ya madai yake ili kuwezesha madai hayo kuchukuliwa ni madai madogo chini ya Kanuni hizi.

(3) Endapo mdai ameacha sehemu ya madai, au kwa kudhamiria, amesamehe sehemu ya madai, hataweza kudai sehemu ya madai iliyoachwa au kusamehewa.

Kukataliwa kwa hati ya madai

6. Hati ya madai itakataliwa endapo-

(a) haioneshi msingi wa madai; au

(b) madai yanazuiwa na sheria nyingine yoyote:

Isipokuwa, mahakama inaweza kumruhusu mdai kurekebisha hati ya madai kwa masharti ambayo itaona yanafaa endapo itajiridhisha kwamba, mdai akiruhusiwa kufanya marekebisho hayo, hati ya madai itabainisha msingi wa madai au dai husika halitaendelea kuzuiwa na sheria yoyote.

Shauri kupangwa kwa hakimu

7. Ndani ya saa ishirini na nne baada ya kufunguliwa kwa madai, hakimu mfawidhi wa mahakama au hakimu anayekaimu nafasi hiyo atapanga shauri husika kwa hakimu kwa ajili ya kutajwa au kusikilizwa.

Upelekaji wa hati ya madai

8.-(1) Mdai atampelekea mjibu madai nakala ya hati ya madai ndani ya siku saba baada ya kufunguliwa kwa madai kwa-

(a) rejesta au kielektroniki;

(b) kuwasilisha kwa mjibu madai mwenyewe; au

(c) kuiacha kwenye nyumba anayoishi mjibu madai au eneo ambalo, kwa kawaida mjibu madai anaishi au kufanya biashara.

(2) Hati ya madai inayotajwa katika kanuni ndogo ya (1) itaambatishwa na notisi inayoshabihiana kwa kadri iwezekanavyo na fomu B iliyopo katika Jedwali la kanuni hizi.

(3) Kwa madhumuni ya kanuni ndogo ya (1), taarifa ya kupokelewa kwa nyaraka kielektroniki au kiapo cha upelekaji wa nyaraka ambacho kinashabihiana kwa kadiri iwezekanavyo na Fomu C iliyoanishwa kwenye Jedwali vitachukuliwa kama uthibitisho wa upelekaji wa nyaraka husika.

Kushindwa kupeleka hati ya madai

9.-(1) Endapo mdai ameshindwa kupeleka hati ya madai chini ya kanuni ya 8, madai hayo yatachukulika kuwa yametelekezwa na yatafutwa.

Majibu ya hati ya madai

Sura ya 11.

10.-(1) Baada ya kupokea hati ya madai, ndani ya siku kumi na nne, mjibu madai atawasilisha mahakamani majibu ya madai yanayoshabihiana kwa kadri iwezekanavyo na Fomu D iliyoainishwa katika Jedwali la Kanuni hizi na atampelekea mdai nakala ya majibu hayo.

(2) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (1), mjibu madai anaweza-

(a) kumlipa mdai mwenyewe kiasi chote kinachodaiwa au kukipeleka mahakamani;
(b) kukubali kiasi chote au sehemu ya kiasi kinachodaiwa na kupendekeza utaratibu wa malipo kwa masharti ambayo wadaawa wanaweza kukubaliana na kuwasilisha mbele ya mahakama makubaliano juu ya pendekezo hilo, kadri mahakama itakavyoelekeza;
(c) kukataa madai yote au sehemu ya madai hayo;
(d) kuibua madai kinzani; au
(e) kuomba kuunganishwa kwa mdaawa mwingine, ambaye mjibu madai anasababu za kuamini kuwa anatakiwa kujibu madai ya mdai.

Majibu ya madai kinzani

11. Mjibu madai ambaye amepelekewa majibu ya hati ya madai na madai kinzani anaweza kuchukua moja au zaidi ya hatua zifuatazo –
(a) kulipa kiasi chote kinachodaiwa kwenye madai kinzani kwa mjibu madai mwenyewe au kuwasilisha kiasi hicho mahakamani,
(b) kukubali kiasi chote kinachodaiwa au sehemu ya kiasi hicho na kupendekeza utaratibu wa malipo kwa masharti ambayo wadaawa wanaweza kukubaliana na kuwasilisha mbele ya mahakama makubaliano juu ya pendekezo hilo; au
(c) kukana madai kinzani yote au sehemu yake.

(2) Mjibu madai aliyechukua hatua yoyote chini ya kanuni ndogo ya (1) (c) atawasilisha majibu ndani ya siku saba baada ya kupokea majibu ya madai na madai kinzani yanayoshabihiana kwa kadiri iwezekanavyo na Fomu E ilivyoainishwa katika Jedwali la Kanuni hizi.

Kushindwa kuwasilisha majibu ya hati ya madai

12.-(1) Endapo mjibu madai ameshindwa kuwasilisha majibu ndani ya muda ulioainishwa, mahakama itatoa amri upande mmoja ya kusikiliza madai.

(2) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (1) mahakama inaweza, ndani ya siku kumi na nne baada ya kutoa amri ya kusikiliza shauri upande mmoja na baada ya mjibu madai kutoa sababu za msingi, kutengua amri hiyo.

Maridhiano kwenye madai

13.-(1) Wadaawa wanaweza kukubaliana kumaliza madai yao kwa maridhiano wakati wowote kabla ya hukumu.

(2) Maridhiano ya madai yatakuwa kwa maandishi na yatasainiwa na wadaawa.

(3) Maridhiano ya madai yatawasilishwa mahakamani na baada ya kuidhinishwa, mahakama itaweka kumbukumbu ya makubaliano hayo, na itatoa tuzo kulingana na makubaliano hayo.

(4) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), (2) na (3) ya kanuni hii, endapo wadaiwa wamekubaliana kwa mdomo kumaliza mgogoro wao, mahakama itaandika makubaliano hayo na kuwataka wadaawa kusaini makubaliano hayo.

## SEHEMU YA TATU
## USIKILIZWAJI WA MASHAURI

Kuhudhuria na madhara ya kushindwa kuhudhuria mahakamani

14.-(1) Kuhudhuria kwa wadaawa kunaweza kufanywa na mdaawa mwenyewe, mwakilishi anayetambulika au wakili aliyeteuliwa kumwakilisha mdaawa au, pale ambapo Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni mdaawa, na afisa wa umma aliyeidhinishwa kwa ajili hiyo.

(2) Endapo mdai hajahudhuria mahakamani katika tarehe iliyopangwa kwa ajili ya usikilizwaji, mahakama inaweza kutupilia mbali madai hayo isipokuwa kama itaona inafaa, kuahirisha usikilizwaji huo.

(3) Endapo mjibu madai hajahudhuria mahakamani katika tarehe iliyopangwa kwa usikilizwaji, baada ya uthibitisho wa upelekaji wa taarifa, mahakama inaweza kusikiliza upande mmoja wa shauri na kutoa hukumu.

(4) Endapo hakuna upande wowote uliohudhuria, mahakama itatupilia mbali madai.

Kutengua hukumu ya upande mmoja na amri ya kutupilia mbali shauri

15.-(1) Endapo madai yametupiliwa mbali chini ya kanuni ya 14(2) au hukumu ya upande mmoja imetolewa chini ya kanuni ya 14(3), mdaawa asiyeridhika anaweza, ndani ya siku 14 baada ya kutolewa kwa amri au hukumu husika, kuiomba mahakama kutengua amri hiyo.

(2) Mahakama inaweza, ikiwa mleta maombi ametoa sababu za msingi, kutengua amri ya kufuta shauri au maamuzi yaliyotolewa ya upande mmoja.

Usikilizwaji wa shauri

16.-(1) Madai yaliyofunguliwa kwa mujibu wa Kanuni hizi yatasikilizwa na kuamuliwa ndani ya miezi mitano tangu kufunguliwa kwake:

Isipokuwa, katika mazingira ya kipekee, mahakama inaweza kuongeza muda usiozidi siku thelathini.

(2) Utaratibu wa usikilizaji na kudodosa mashahidi hautakuwa rasmi kwa lengo la kutoa haki ya msingi kwa wakati.

(3) Endapo pande zote mbili zimehudhuria, mdai atafungua shauri kwa kuita mashahidi kama wapo, ambao wanaweza kuhojiwa na wadaawa.

(4) Baada ya mdai kufunga ushahidi wake, mjibu madai atawasilisha utetezi wake, maelezo kuhusu ushahidi wa madai kinzani, kama upo na anaweza kuita mashahidi ambao wanaweza kudoswa na mdai.

(5) Mahakama inaweza kutoa wito kwa shahidi yoyote kuhudhuria na itakuwa na mamlaka ya kulazimisha uhudhuriaji kwake mahakamani.

(6) Ushahidi utatolewa kwa mdomo chini ya kiapo au uthibitisho, au kwa hati ya kiapo:

Isipokuwa, shahidi anayetoa ushahidi kwa hati ya kiapo anaweza kuitwa kwa ajili ya kudodoswa pale atakapohitajika na mahakama au upande mwingine.

(7) Isipokuwa kwa amri ya mahakama, hakuna mdaiwa atakayepata fursa ya kutoa maelezo baada ya usikilizwaji wa shauri kufungwa isipokuwa kwa idhini ya mahakama.

Katazo la maahirisho

17. Endapo usikilizaji umeanza, mashahidi wote waliofika mahakamani kutoa ushahidi katika shauri husika watadodoswa, isipokuwa kama mahakama, kwa sababu zitakazoandikwa, itaona kuna sababu za kuahirisha usikilizaji wa shauri hilo.

## SEHEMU YA NNE
## HUKUMU NA UTEKELEZAJI WA TUZO

Hukumu na tuzo

18. Mahakama itatoa hukumu na tuzo ndani ya siku thelathini baada ya kukamilika kwa usikilizwaji wa shauri.

Gharama
Sura ya 33.

19. Gharama za uendeshaji wa mashauri chini ya Kanuni hizi zitazingatia masharti yaliyowekwa na Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Madai.

Utekelezaji wa tuzo
Sura ya 33

20. Tuzo iliyotolewa chini ya Kanuni hizi itatekelezwa kwa utaratibu uliowekwa chini ya Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Madai.

## SEHEMU YA TANO
## RUFAA NA MAPITIO

Utaratibu wa rufaa na mapitio

21.-(1) Mdaawa yeyote ambaye hajaridhika na amri au uamuzi wa mahakama chini ya Kanuni hizi, anaweza kukata rufaa Mahakama Kuu.

Sura ya 11
Sura ya 33

(2) Rufaa na mapitio chini ya kanuni hizi zitasimamiwa na sheria zinazosimamia rufaa na mapitio katika mahakama za Hakimu Mkazi na Mahakama za Wilaya.

## SEHEMU YA SITA
## MASHARTI YA JUMLA

Namna ya kuwasilisha maombi

22.-(1) Kila maombi mbele ya mahakama chini ya Kanuni hizi yatawasiliswa kwa mdomo wadaawa wakiwepo, yatasikilizwa na kuamuliwa siku hiyo hiyo isipokuwa kama mahakama itaamua, pale ambapo haki inahitaji, kuruhusu maombi yafanyike kwa maandishi kwa njia ya hati ya faragha iliyoambatishwa na kiapo.

(2) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (1), maombi chini ya kanuni ya 12 na 15 ya Kanuni hizi yatakuwa kwa maandishi kwa njia ya hati ya faragha iliyoambatishwa na hati ya kiapo.

Ada
TS 247 la Mwaka 2018

23. Masharti ya Kanuni za Ada za Mahakama za Mwaka 2018 yatatumika kwa ada zinazolipwa chini ya Kanuni hizi.

FOMU A

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

JEDWALI

KATIKA MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI/WILAYA YA.........................
INAYOKETI........................

SHAURI LA MADAI MADOGO NA............ LA................

...................................................... MDAI

DHIDI YA

..................................................... MJIBU MADAI

HATI YA MADAI
*(Imetengenezwa chini ya kanuni za 5(1),8(2), 10(1) na 11(2))*

1. Jina kamili..........................................................................................................mdai*
Hadhi ya kisheria ya mdai (*weka alama ya vema panapostahili* )
□ mtu binafsi □ umiliki pekee □ ubia □ kampuni □ chama cha ushirika □ Serikali □ aina nyingine (*taja)*
Anwani ya makazi.........................................................................................................
Anwani ya biashara na posta.........................................................................................
Msimbo wa posta...........................................................................................................
Nambari ya simu..........................................................................................................
Barua pepe....................................................................................................................

na

2. Jina kamili.......................................................................................... Mjibu Madai*
Hadhi ya kisheria ya mjibu madai (*Weka alama ya vema panapostahili* )
□ mtu binafsi □ umiliki pekee □ ubia □ kampuni □ chama cha ushirika □ Serikali □
Aina nyingine (*taja)*
Anwani ya makazi.........................................................................................................
Anwani ya biashara na posta.........................................................................................
Msimbo wa posta...........................................................................................................
Nambari ya simu..........................................................................................................
Barua pepe....................................................................................................................

**Iwapo kuna mdai au mjibu madai zaidi ya mmoja toa maelezo ya kila mdai au mjibu madai*

3. Asili ya madaina msingi wake (*weka alama ya vema panapostahili* )

□ Urejeshaji wa madeni
□ Riba ya Serikali kwa mujibu wa hukumu au sheria
□ Urejeshaji wa deni lolote la madai linalotokana na mkataba
□ Asili au msingi mwingine madai (*taja kwa kifupi*)..........................................................
..............................................................................................................................
..............................................................................................................................

4. Tarehe ya msingi au chanzo cha madai:........................................

5. Eleza kwa ufupi mazingira ambayo madai yalitokea, na kuambatisha nyaraka zinazounga mkono madai yako (*kama zipo*)

*Tangazo la Serikali Na. 167 (Linaendelea)*
..........................................................................................................................................
..........................................................................................................................................

6. Nafuu zinazoombwa; (*weka alama ya vema panapostahili* )
□ Tuzo ya kiasi cha jumla ya shilingi ............................
□ Fidia
□ Gharama za madai (*zitakazo kadiriwa na mahakama*)
□ Nafuu zingine stahiki (*eleza kwa kifupi*)...........................................................................................
..........................................................................................................................................

7. Jaza sehemu hii kama kiasi kinazidi kiwango cha madai madogo.
Kwa kufungua madai haya, mimi ............................................................................ (mdai) ninaacha na kusamehe kiasi cha shilingi ..............................................., bila kujumlisha gharama na riba.

........................
saini ya mdai

UTHIBITISHO

Nathibitisha kwamba taarifa iliyotolewa hapa juu ni ya kweli.

...........................
saini ya mdai

Imethibitishwa hapa.............*(mahali)* leo tarehe ...............mwezi.............mwaka 20................

...........................
saini ya mdai

Imewasilishwa kwa ajili ya kufunguliwa tarehe....................................

Imesainiwa..............................................
afisa masijala

FOMU B

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA

KATIKA MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI/WILAYA YA........................
INAYOKETI.......................

SHAURI LA MADAI MADOGO NA........... LA................

..................................................... MDAI

DHIDI YA

.................................................... MJIBU MADAI

NOTISI KWA MJIBU MADAI

*(Imeandaliwa chini ya kanuni ya 8(2))*

Kwa …………………………………………
…………………………………………

KWA KUWA mdai tajwa hapo juu amefungua shauri la madai dhidi yako ambalo maelezo yake yamebainishwa kwenye nakala ya hati ya madai iliyo ambatishwa;

UNA TAARIFIWA KWAMBA**,** unalazimika kuwasilisha majibu ya hati ya madai katika nakala mbili ndani ya siku kumi tokea tarehe ya kupokea notisi hii. Kama kuna mdai zaidi ya mmoja, idadi ya nakala za nyongeza zinazotosheleza kumpelekea kila mdai zitawasilishwa. Kama kuna wadai wazaidi ya mmoja na majibu siyo ya pamoja, unatakiwa kuwasilisha nakala za kumtosha kila mdaiwa.

NA UFAHAMU KWAMBA iwapo hutawasilisha majibu ya hati ya madai ndani ya muda ulioelezwa, mahakama inaweza kuendelea kusikiliza shauri upande mmoja na kutoa hukumu dhidi yako.

PIA UFAHAMU KWAMBA shauri limepangwa kwa ajili ya kutolewa amri mbele ya Mhe…………………..hakimu, tarehe………mwezi……… mwaka 20…..., saa…….. kamili asubuhi/mchana.

IMETOLEWA KWA MKONO WANGU NA MUHURI WA MAHAKAMA
leo tarehe…………mwezi………20…………

**…………………………**
hakimu
(lakiri/muhuri)

KUKIRI UPOKEAJI WA HATI YA MADAI

Mimi…………………………………………….ninakiri kupokea nakala ya notisi hii leo tarehe…………….mwezi……………. 20 ……..

**……………………..**
mdaiwa

FOMU C

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA

KATIKA MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI/WILAYA YA........................
INAYOKETI.......................

SHAURI LA MADAI MADOGO NA........... LA...............

..................................................... MDAI

DHIDI YA

.................................................... MJIBU MADAI

KIAPO CHA KUPELEKA HATI YA MADAI

*(Kimetengenezwa chini ya kanuni ya 8(3))*

Mimi.................................................................... ninaapa /ninathibitisha kwamba-
(1) Mimi ni................................................(*taja wadhifa)*
(2) Mnamo tarehe...................................., nilipokea hati ya madai iliyotolewa na mahakama hii ya ......................................................... katika shauri la madai madogo namba .....................la .................. katika mahakama tajwa tarehe...................................... kwa ajili ya kumpelekea ...................................................................
(3) Mjibu madai huyo .......................................................... ambaye ninamfahamu/ametambulishwa kwangu na .......................................................................ambaye ninamfahamu na nilimpelekea hati ya madai tarehe ............................................ majira ya ....................*mchana/alasiri kwa kumpa nakala yake na kumtaka atie saini kwenye hati ya madai halisi ya madai au mjibu madai huyo........................................... amekataa kutia saini mbele ya ........................................................................ (shahidi) au
...............................................................................................................................................
...............................................................................................................................................
Imeapwa/imethibitishwa na................................................ambaye ninamfahamu/ametambulishwa kwangu na.............................................ambaye ninamfahamu leo tarehe .............mwezi....................mwaka 20.....
Mbele ya:.................................................................. saini...................................................................
Anwani.......................................................................................................................................

...............................................
kamishna wa viapo

*(Toa sababu nyinginezo za kutokupokelewa kwa hati ya madai/futa isiyohusika)*

FOMU D

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA

KATIKA............................ YA..................

KATIKA MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI/WILAYA YA........................
INAYOKETI.......................

SHAURI LA MADAI MADOGO NA........... LA................

..................................................... MDAI

DHIDI

..................................................... MJIBU MADAI

MAJIBU YA HATI YA MADAI

*(Imetengenezwa chini ya kanuni ya 10(1))*

1. Jina kamili............................................ mjibu madai
   Hadhi ya kisheria ya mjibu madai (*weka alama ya vema panapostahili* )
   □ mtu binafsi □ umiliki pekee □ ubia □ kampuni □ chama cha ushirika □ Serikali □ aina nyingine (*taja)*
   Anwani ya makazi.........................................................................................................
   Anwani ya biashara na posta....................................................................................
   Msimbo wa posta..........................................................................................................
   Nambari ya simu.........................................................................................................
   Barua pepe....................................................................................................................

2. Majibu ya hati ya madai

Katika kujibu hati ya madai ya tarehe.....................................najibu kama ifuatavyo: (*weka alama ya vema panapostahili* )
□ Mjibu madai hadaiwi na mdai kiasi chochote
□ Mjibu madai anadaiwa na mdai kiasi cha shilingi...........................tu kati ya kiasi kinachodaiwa katika hati ya madai. (*taja kiasi kilichokubaliwa*)
□ Mjibu madai anakiri madai yote ya mdai
□ Mjibu madai amelipa kwa mdai kiasi chote kinachodaiwa katika hati ya madai
□ Mdai ndiye anayedaiwa na mjibu madai kiasi cha shilingi...................................kutokana na ...............................................................(*eleza msingi wa madai ya kiasi kinachodaiwa dhidi ya mdai*)
□ Iwapo majibu yanakanusha madai yote au sehemu ya madai, toa sababu kwa nini madai hayo yanakataliwa (*eleza kwa kifupi*)
..........................................................................................................................................................
..............................................................................................................................

3. Madai kinzani
Bila kuathiri majibu ya mjibu madai katika aya ya pili, mjibu madai anawasilisha madai kinzani ya jumla ya shilingi............................................................dhidi ya mdai kwa msingi kwamba
.............................................................................................................................................(*Taja kiasi na msingi wa madai kinzani*)

*Tangazo la Serikali Na. 167 (Linaendelea)*

4. Kukata deni

Pamoja na kukubali madai ya mdai kwa jumla ya kiasi cha shilingi..................................................
mjibu madai anadai haki ya kukataa deni kwa jumla ya shilingi.....................kwa msingi kwamba
..........................................................................................................................................
......................................................................................................................................
(*Taja kiasi na sababu za kukata deni*)

5. Nafuu zinazoombwa

Mjibu maombi anaomba mahakama: (*weka alama ya vema panapostahili)*

□ Madai yatupiliwe mbali kwa gharama.

□ Hukumu itolewe kwa upande wa mjibu madai dhidi ya mdai kwa kiasi cha shilingi

□ Hukumu itolewe kwa upande wa mjibu madai dhidi ya mdai kwenye madai kinzani au madai ya kukata deni kiasi cha shilingi............................................

UTHIBITISHO

Ninathibitisha kwamba taarifa iliyotolewa hapo juu ni ya kweli.

................................
saini ya mjibu madai

Imethibitishwa hapa.................*(mahali)* leo tarehe ............mwezi.................mwaka 20...........

...........................
saini ya mjibu madai

Imewasilishwa kwa ajili ya kufunguliwa tarehe...................................

imesainiwa..............................................
afisa masijala

**(Futa isiyohusika)*

KUKIRI UPOKEAJI

Ninakiri kupokea majibu ya hati ya madai iliyowasilishwa kwangu, pamoja na nyaraka zilizoambatishwa leo tarehe .......................................................

.....................
saini ya mdai

FOMU E

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA

KATIKA MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI/WILAYA YA........................
INAYOKETI.......................

SHAURI LA MADAI MADOGO Na........... LA...............

..................................................... MDAI

DHIDI

.................................................... MJIBU MADAI

MAJIBU YA MADAI KINZANI

*(Imetengenezwa chini ya kanuni ya 11)*

1. Katika kujibu madai kinzani ya tarehe.....................................najibu kama ifuatavyo: (*weka alama ya vema panapostahili* )

□ Mdai hadaiwi na mjibu madai kiasi chochote

□ Mdai anadaiwa na mjibu madai kiasi cha shilingi........................... tu kati ya kiasi kinachodaiwa katika hati kinzani ya madai

□ Mdai anakiri madai yote ya mjibu madai

□ Mdai amelipa kwa mjibu madai kiasi chote kinachodaiwa katika madai kinzani

□ Mjibu madai ndiye anaye daiwa na mdai kiasi cha shilingi. .....................................kutokana na .................................................................................................(*eleza msingi wa madai ya kiasi kinacho daiwa dhidi ya mdai*)

□ Mdai anakana madai kinzani kwa sababu zifuatazo *(eleza kwa ufupi iwapo madai yamekanushwa)*
.....................................................................................................................................................
..................................................................................................................

2. Maombi

Mdai anaomba mahakama: (*weka alama ya vema panapostahili)*

□ Madai kinzani/kukata deni yatupiliwe mbali kwa gharama

□ Hukumu itolewe kwa upande wa mdai dhidi ya mjibu madai kwa kiasi cha shilingi

□ Hukumu itolewe kwa upande wa mdai dhidi ya mjibu madai kwenye hati ya madai kiasi cha shilingi...........................................

UTHIBITISHO

Ninathibitisha kwamba taarifa iliyotolewa hapo juu ni ya kweli.

................................
saini ya mdai

Imethibitishwa hapa................*(mahali)* leo tarehe ...........mwezi................mwaka 20..........

..........................
saini ya mdai

Imewasilishwa kwa ajili ya kufunguliwa leo tarehe ...........mwezi................mwaka 20..........

imesainiwa..............................................
afisa masijala

*(Futa isiyohusika)*

KUKIRI UPOKEAJI

Ninakiri kupokea majibu ya madai kinzani yaliyowasilishwa kwangu pamoja na nyaraka zilizoambatishwa leo tarehe ...........mwezi................mwaka 20..........

..................................
saini ya mjibu madai

Dar es Salaam,
27 Februari, 2023

IBRAHIM HAMIS JUMA
*Jaji Mkuu*

*Tangazo la Serikali Na. 167 (Linaendelea)*